



**Yerusalemu Mpya**

**Makanisa Ulimwenguni Kote**

**Mchungaji Tony Alamo**

**Taifa la Kikristo la Alamo**

**Toleo 18800**

# KRISMASI NI WOKOVU

**na Tony Alamo**

Ilikuwa miezi tisa kabla ya siku ya Krismasi ya kwanza, kuzaliwa kwa KRISTO. MUNGU alikuwa, kama kawaida, ameketi kwenye kiti CHAKE cha enzi MBINGUNI.<sup>1</sup> “NAYE [malaika wa BWANA] akanionyesha [Yohana, mtume] mto wa maji ya UZIMA, wenyewe kung’aa kama bilauri.” Mwanzo 1:7 inasema, “MUNGU akalifanya anga [ambalo ni kitenganishi kati ya maji ya mbingu na maji ya nchi], akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga [maji haya yaliyo juu ya anga ni ROHO MTAKATIFU, maji ya UZIMA, ambayo MUNGU huyapeleka kwa kila aaminiye katika KRISTO<sup>2</sup>]: na ika-wa hivyo [na bado iko hivyo].”

Tena, hayajachafuliwa hata kidogo, bali ni halisi na “kung’aa kama bilauri, yakitoka katika kiti cha enzi cha

MUNGU, na cha MWANA-KONDOO. Katikati ya njia kuu yake, na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa UZIMA, uzao matunda, aina kumi na mibili, wenyewe kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa” (Ufunuo 22:1-2).

Mto huu, uliomtunga YESU katika tumbo la Mariamu, ni mto ule ule ambao hatimaye utamzaa KRISTO na BABA kwa ROHO kwa kila muumini atakayeaminu katika KRISTO.<sup>3</sup> ROHO huyu huyu ni mto ambao utamfufua kila moja kutoka wafu katika siku ya mwisho,<sup>4</sup> wengine kwa UZIMA wa milele, na wengine kwa aibu ya milele na hukumu (Danieli 12:2, Ufunuo 20:6).

Ufunuo 14:10-11 inazungumzia wale ambao watapata hukumu ya milele: “Yeye naye atakunywa katika



*Mchungaji Alamo na marehemu mkewe Susan katika kipindi chao cha kimataifa cha televisheni. Picha - 1974*

mvinyo wa ghadhabu ya MUNGU, iliyotengenezwa pasipo kuchanganya-wa na maji, katika kikombe cha hasira YAKE; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za MWANA-KONDOO: Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele: wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujiduo huyo mnyama [mnyama ni Umoja wa Mataifa wa Vatican, serikali moja ya dunia, iitwayo Mpango Mpya wa Dunia, uliotungwa na Cecil Rhodes] na sanamu yake, na kila

*(Inaendelea ukurasa wa 2)*

<sup>1</sup> 1 Fal. 22:19, Zab. 2:4, 9:4, 11:4, 47:8, 103:19, Isa. 6:1, 66:1, Dan. 7:9-10, Mat. 5:34-35, 23:21-22, Mdo. 7:48-49, Ufu. 4:2-6, 9-10, 5:1, 6-7, 13, 6:16, 7:9-11, 15, 17, 12:5, 16:17, 19:4-5, 20:11, 21:5, 22:1, 3 <sup>2</sup> Yoh. 3:5-6, 4:7-14, 7:37-39, Efe. 5:25-27, Ebr. 10:21-23, 1 Yoh. 5:5-8, Ufu. 21:6 <sup>3</sup> Eze. 36:27, Yn 4:13-14, 14:15-26, 15:1-11, 26, 16:7-14, 17:20-23, 26, 1 Kor. 3:9, 16-17, 6:19-20, 2 Kor. 6:16-18, Gal. 2:20, Efe. 2:18-22, Fil. 2:12-13, Kol. 1:27-29, 2 Tim. 1:14, Ufu. 21:6, 22:17 <sup>4</sup> Ayu. 19:25-27, Zab. 17:15, 49:15, Dan. 12:1-3, Hos. 13:14, Mat. 3:11-12, 8:11-12, 13:24-43, 25:30-46, Yoh. 5:21-29, 6:39-54, 11:23-27, Mdo. 24:14-15, Rum. 8:10-23, 1 Kor. 6:14, 15:35-54, 2 Kor. 4:14, Ufu. 20:11-15, 21:8

## KRISMASI NI WOKOVU

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)

aipokeaye chapa ya jina lake.” Mtu ye yote atakayejihusisha na serikali hii mbaya ya kishetani, ambayo MUNGU anaichukia, atapaswa kutubia haraka dhambi hii, kisha azaliwe tena kwa ROHO, mto wa UZIMA, na aenze kumtumikia BWANA.

Tena, MUNGU alikuwa akijiandaa kumtuma MWANAWE wa pekee kutoka kiti cha enzi cha MUNGU ndani ya tumbo la Mariamu, kwa ROHO MTAKATIFU, mto wa UZIMA, kuwa MUNGU-MWANADAMU wa kwanza (Adamu wa mwisho). “Ndiyivo ilivyoandikwa, Mtu wa kwanza, Adamu, akawa nafsi iliyo hai; Adamu wa mwisho ni ROHO yenye kuhuisha [ITOAYO-UZIMA]” (1 Wakorintho 15:45). Hii ilikuwa kuwapa wandalamu wote nafasi ya pili kuokoka kutoka kwenye maisha ya dhambi, kutoka kwenye mtego wa Shetani, na kutoka kwenye Jehannamu ya milele, katika Ziwa la Moto na Kiberiti.<sup>5</sup>

KRISTO, ambaye ni NENO la MUNGU, ilimpasa kuzaliwa katika mwili kwa namna tofauti kuliko mtu yeyote yule. ATAKUWA mwanadamu, tena ATAKUWA asiyé na dhambi kwa sababu ALIZALIWA kwa uwezo wa ROHO MTAKATIFU, mto wa UZIMA kutoka kwenye kiti cha enzi cha MUNGU aliye hai.<sup>6</sup> Ilimpasa MASIHI WA MUNGU kushuka kutoka mbinguni kuwa MWANA wa MUNGU ndani ya tumbo la binti mdogo bikira.<sup>7</sup> Kihistoria Mariamu alijulikana kuwa na umri wa kati ya miaka 9 au 10 wakati wa utungwaji wa mimba safi isiyo na mawaa ya YESU tumboni mwake.

Kulikuwa na kumiminwa kwa ROHO MTAKATIFU WA MUNGU wakati ule katika dunia yote ambaye

Wapendwa Huduma za Tony Alamo, Bwana asifiwe. Natumaini u mzima katika Kristo. Nafurahi sana kushiriki uzoefu wangu katika Mungu na ziara yangu ya Injili. Siku kwa siku tunakua katika Kristo na ku-wafanya watu kukua katika Mungu wetu. Hivi karibuni timu yetu ya Alamo ilienda kwenye ziara ya Injili na ikafanikiwa kueneza Injili. Baadhi ya mipango yetu imewekewa pin-gamizi na Shetani na akatengeneza baadhi ya matatizo ya kifedha, lakini tuliyashinda kwa maombi. Miujiza mingi imefanya na Roho Mtakatifu wa Mungu. Mtu mmoja kanisani katika maisha yake ya zamani alijenga mahekalu ya miungu na sanamu, lakini sasa amebadilishwa kwa Yesu. Anakuja kanisani mara kwa mara na amekuwa mtu wa maombi. Tunasambaza maandiko yetu na ushuhuda wa Mchungaji wetu Tony Alamo kwa watu

amedumu hadi leo hii. Kumiminwa huku kwa ROHO MTAKATIFU kulikuwa kumetabiriwa na nabii Yoeli katika Yoeli 2:28-31: “Hata itakuwa baada ya hayo, ya kwamba nitamimina ROHO YANGU juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumiishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, nitamimina ROHO YANGU. Nami nitaonyesha mambo ya ajabu katika mbingu na katika dunia, damu, na moto, na minara ya moshi. Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla hajaja hiyo siku ya BWANA iliyo kuu na itishayo.” Kila mtu alikuwa akitarajia MASIHI WA MUNGU kuonekana katika tukio la wakati ule.

YESU alikuwa mwanadamu wa kwanza kuzaliwa kwa mto wa UZIMA

## India

wengi sana. Inahamasisha sana watu kumjua Yesu.

Asante sana kwa kunipa fursa kue-neza Injili pamoja nawe. Watu wengi wananiulizia fasihi zaidi na maandiko ya kusambaza. Nashangazwa na miujiza ya Mungu.

Tunamwombea Mchungaji Alamo aachiliwe haraka. Katika sala zetu za kila siku, tunaomba kwamba aachiliwe katika jina la Mungu anayejua kila jambo. Haachi watu wake. Tupo hapa kulifanya Neno Lake llijulikane. Kitu pekee tulicho nacho katika dunia hii ni Neno la Mungu. Halishindwi, hivyo tusipoteze imani, na tusilikate Neno la Mungu.

Tafadhali nitumie maandiko na vitabu. Itahamasisha timu yetu kufanya mambo mema zaidi kwa Mungu. Bwana Asifiwe. Tuma maandiko zaidi na Biblia kuhamasisha timu. Asante.

Darakonda Sagar  
Andhra Pradesh, India

MA (ROHO MTAKATIFU). Ili kila mmoja aokoelewe au aendelee kuo-kolewa na kwa ROHO MTAKATIFU, ni lazima anywe maji ya mto wa UZIMA na ale matunda ya mti wa UZIMA mara zote kila siku.<sup>8</sup> Ni lazima pia ale majani ya mti wa UZIMA kila siku kwa ajili ya uponyaji wa matalifa, au atakufa hakika.

Katika Mwanzo 2:17, MUNGU alisema kwamba siku utakapokula matunda ya ujuzi wa mema na mabaya (ulimwengu), “hakika utakufa.” Usipokula matunda ya mti wa UZIMA na kunywa katika mto wa UZIMA mara zote kila siku, kwa hakika unakula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya, jambo linalo-maanisha utakufa hakika. Neno hili latoka kwa MUNGU, na MUNGU hawezni kudanganya.<sup>9</sup> Waembrania 6:18 anathibitisha ukweli huu, akisema “ili kwa vitu viwili visivyoweza

<sup>5</sup> Lk. 24:46-47, Yn 12:23-24, Mdo. 26:15-18, Rum. 5:6-21, 8:32-34, 1 Kor. 15:45-57, Gal. 4:4-5, Efe. sura ya. 2, Kol. 1:12-14, 1 Thes. 1:9-10, Ebr. 9:13-15, 1 Pet. 1:3-5, Ufu. 1:18 <sup>6</sup> Isa. 7:14-15, Rum. 8:3, Fil. 2:6-8, Ebr. 2:16-18, 4:14-15, 5:8-9, 7:26-28, 9:14, 1 Pet. 1:18-19, 2:22, 1 Yoh. 3:5-6, Ufu. 5:1-10 <sup>7</sup> Isa. 7:14, Mat. 1:18-25, Lk. 1:26-37 <sup>8</sup> Kum. 8:3, Yos. 1:8, Isa. 55:1-3, Mat. 4:4, 5:6, 26:26-28, Yoh. 4:10, 14, 6:31-35, 48-58, 63, 7:37-39, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Ufu. 21:6, 22:1-2, 17 <sup>9</sup> Hes. 23:19, Kum. 7:9-10, 32:4, Yos. 23:14-16, 1 Sam. 15:29, Zab. 36:5, 89:34, 100:5, 105:7-10, Yoh. 17:17, Rum. 3:4, 1 Thes. 5:24, 2 Tim. 2:13, Tit. 1:1-2, Ebr. 6:10-19



*Mchungaji Karumanchi  
Prakasaraao na timu yake  
wakisambaza maandiko ya  
Injili ya Mchungaji Alamo  
katika eneo la Ramanakkapeta,  
Andhra, South India.*

kubadilika, ambavyo katika hivyo MUNGU hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyo imara, sisi tulio-kimbilia kuyashika matumaini yale yawekwayo mbele yetu.” Vitu viwili visivyobadilika ni kwamba ni lazima tule matunda ya mti wa UZIMA mara zote kila siku na tunywe katika mto wa UZIMA, amba ni ROHO MTAKATIFU, mara zote kila siku.

Isaya 7:14 inasema, “Kwa hiyo BWANA MWENYEWE atawapa ishara; Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa MTOTO MWANAMUME, NAYE atamwita jina LAKE IMANUEL.” Na tena, Isaya 9:6 inasema, “Maana kwa ajili yetu MTOTO amezaliwa, tumepewa MTOTO MWANAMUME: na uweza wa kifalme utakuwa begani MWAKE: naye ataitwa jina LAKE, MSHAURI WA AJABU, MUNGU MWENYE NGUVU, BABA WA MILELE, MFALME WA AMANI.”

“Mwezi wa sita, malaika Gabrieli alitumwa na MUNGU kwenda mpara mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, Kwa mwanamwali bikira ali-

yekuwa ameposwa [amechumbiwa] na mtu [mtu aliyekomaa komyaka], jina lake Yusufu, wa mbari ya Daudi; na jina lake bikira huyo ni Mariamu. Akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu, uliyepewa neema, BWANA yu pamoja nawe. Naye akafadhai-ka sana kwa ajili ya maneno yake, akawaza moyoni, Salamu hii ni ya namna gani? Malaika akamwambia, Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa MUNGU. Tazama, utachukua mimba na kuzaa MTOTO MWANAMUME; na jina LAKE utamwita YESU. HUYO atakuwa mkuu, ataitwa MWANA wa ALIYE JUU: na BWANA MUNGU ATAMPA kitu cha enzi cha Daudi, baba YAKE: ATAIMILIKI nyumba ya Yakobo hata milele: na ufalme wake utakuwa hauna mwisho.

“Mariamu akamwambia malaika, Litakuwaje neno hili, maana sijui mume? Malaika akajibu akamwambia, ROHO MTAKATIFU atakujilia juu yako, na nguvu zake ALIYE JUU zitakufunika kama kivuli: kwa sababu hiyo hicho KITAKATIFU kita-

kachozaliwa kitaitwa, MWANA wa MUNGU” (Luka 1:26-35).

Kulikuwa na nabii nyingine 333 zinazohusu ujio wa kwanza wa KRISTO ambazo zilitimilizwa siku ya Krismasi na katika MAISHA YAKE yote.<sup>10</sup> Watu wengi wa dunia walikuwa na uelewaji wa nabii chache kati ya hizi. Hata mwovu Mfalme Herode alikuja kuelewa kuhusu baadhi ya nabii hizi, kama ule wa KRISTO kuzaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi. Wakti huo, Mfalme Herode “akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta habari kwao, kuhusu alikozaliwa KRISTO. Nao wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi: kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii, Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda, Hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda: Kwa kuwa kwako atatoka mtawala Atakayewachunga watu WANGU Israeli. Kisha Herode akawaita wale mamajusi faraghani, akapata kwao hakika ya

(Inaendelea ukurasa wa 4)

<sup>10</sup> The Messiah According to Bible Prophecy (Masihi kwa Mujibu wa Unabii wa Biblia) na Mchungaji Tony Alamo

## KRISMASI NI WOKOVU

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3)

muda tangu ilipoonekana ile nyota. Akawapeleka Bethlehemu, akasema Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya MTOTO; na mkiisha KUMWONA, nileteeni habari, ili mimi nami niende NIMSUJUDIE. Nao waliposikia maneno ya Mfalme, walishika njia; na tazama, ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo MTOTO. Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno. Wakaingia nyumbani, wakamwona MTOTO pamoja na Mariamu MAMAYE, wakaanguka WAKAMSUJUDIA; nao walipokwisha kufungua hazina zao, WAKAMTOLEA; dhahabu na uvumba na manemane.

“Nao wakiisha kuonywa na MUNGU katika ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwa njia ny ingine. Na hao walipokwisha kwendza zao, tazama, malaika wa BWANA alimtokea Yusufu katika ndoto, akasema, Ondoka, umchukue MTOTO na mama YAKE, ukimbilie Misri, ukae huko hata nikwambie; kwa maana Herode anataka KUMTAFUTA mtoto amwangamize. Akaondoka akamchukua MTOTO na mama YAKE usiku, akaenda zake Misri; akakaa huko hata alipokufa Herode; ili litimie neno lililonenwa na BWANA kwa ujumbe wa nabii, akisema, kutoka Misri nalimwita MWANANGU.

“Ndipo Herode, alipoona ya kuwa amedhihakiwa na wale mamajusi, alighadhhibika sana, akatuma watu wakawaue watoto wote wanaume waliokuwa wako huko Bethlehemu na viungani mwake mwote, tangu wenyе miaka miwili na waliopungua, kwa muda ule aliouhakikisha

kwa wale mamajusi. Ndipo lili potimia neno lililonenwa na nabii Yeremia, akisema, Sauti ilisikiwa Rama, Kilio, na maombolezo mengi, Raheli akiwalilia watoto wake, asi kubali kufarijiwi, kwa kuwa hawako” (Mathayo 2:4-18).

Watu wengi hawampokei KRISTO wala kuendelea katika YEYE kwa hofu ya mateso na dhiki.<sup>11</sup> Mathayo 13:20-21 inasema, “Naye aliyepandwa MBEGU penye miamba [moyo wa jiwe], huyo ndiye alisikiaye lile NENO, aka lipokea mara kwa furaha; lakini hana mizizi ndani yake, bali hudumu kwa muda: ikitukia dhiki au udhia kwa ajili ya lile NENO, mara huchukizwa” – naweza kuongeza, anaogopa. Watu wanaweza kusema, “Oh! Oh! Sikutaka hili! Nilitaka kupata faida na utukufu na zawadi ya wokovu, lakini si hili (udhia na dhiki).” Hivyo wao hu jitenga hutanga mbali na BWANA, na kuishia kwenye Ziwa la Moto milele, ambalo ni bayu zaidi kuliko dhiki na udhia. Sote tunapaswa kumshukuru MUNGU kwamba YESU, Mariamu na Yusufu hawakukimbia kutoka kwenye mateso yao na dhiki.

Siku ya Krismasi, MWOKOZI alizaliwa. Hata zaidi ya MWOKOZI, MUUMBWA wa Mbingu na nchi alizaliwa katika mwili.<sup>12</sup> ALIUMBWA pia jua, mwezi, makundi yote ya nyota, sayari, na nyota, oksijeni, mvutano, kila atomu, na kila molekuli. Yohana 1:3-5 inasema, “Vyote vilifanyika kwa HUYO; wala pasipo YEYE hakikufanyika chochote klichofanyika. Ndani YAKE ndimo ulimokuwa UZIMA, nao ule UZIMA ulikuwa NURU ya watu. Nayo NURU yang’aa gizani [dunia hii ya giza]; wala giza halikuiweza [watu wa kimwili wa dunia hii waliojawa na giza hawawezi kuelewa mambo ya ulimwengu wa kiroho].”

Watu wanapopiga taswira ya KRISTO akiwa ameketi kwenye kitin

CHAKE cha enzi Mbinguni (na ni lazima tupige taswira, vinginevyo tunapotea<sup>13</sup>), twaona mto huu wa maji ya UZIMA “ukitoka katika kiti cha enzi cha MUNGU, na cha MWANA-KONDOO [kiti CHAKE cha enzi]. Katikati ya njia kuu yake, na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwepo mti wa UZIMA [ambao pia ni mfano wa YESU, NENO la MUNGU], uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenyе kutoa matunda yake kila mwezi: na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa” (Ufunuo 22:1-2).

Akili ya mwanadamu haiwezi kabisa kuelewa mambo yote ambayo nguvu ya MUNGU mwenyezi inafanya, hasa yale yote ANAYOFANYA kwa wakati mmoja. Nitaanza kwanza katika kazi YAKE ya kushughulika na majaribu na mateso ya kila mwanadamu, magonjwa yao, maradhi, na udhaifu, furaha yao na huzuni, vizazi vyao na vifo vyao, uponyaji wao, sala zao, utumishi wao na upokezi wa NENO LAKE, vita vyao na matetes ya vita. Tena anashughulika na watu wanaotazamia kuua, kutoa mimba, kujiua, na dhambi ny ingine zote, kama ushoga, uzinzi, usherati, usagaji, na kuzini na wanyama. MUNGU Anafahamu sana kila unyasi, vile vile hata viumbwa wa mmeng’eny wa kila ndege, kila samaki, kila mnyama, na kila mwanadamu. ANAFAHAMU sana hisia za kila mwanadamu na tamaa za kila mtu. Anajua wakati ye yote ANAPOMWEKA pembeni kama vile YEYE si kitu.<sup>14</sup>

Kuna mfano kuhusu hili katika Biblia. Ni mfano wa mbegu ya

13 Mit. 29:18, Mat. 13:10-16, Mdo. 28:27, Rum. 8:24-25, 2 Kor. 9:24-25, Fil. 3:13-15 14 1 Sam. 16:7, 1 Fal. 8:39, 2 Fal. 19:27, 1 Nya. 28:9, Ayu. 31:4, 34:21-22, 25, Zab. 44:21, 50:21-22, 139:1-6, 12-16, Mit. 1:25-33, 15:3, 11, Isa. 42:9, Yer. 16:17, Eze. 11:5, Mat. 6:8, Lk. 16:15, Mdo. 15:18



haradali, ambayo YESU aliiweka mbele ya watu, akisema, "Ufalme wa mbinguni [NENO LA MUNGU] umefanana na punje ya haradali [watu wa dunia hii wanaoliona NENO la MUNGU, Ufalme wa Mbinguni, kuwa si kitu, na mdogo kuliko mambo yote, ndogo kuliko mbegu zote (MANENO)], aliyoitwaa mtu akaipanda katika shamba lake [moyo wake]; Nayu [haradali] ni ndogo kuliko mbegu zote; lakini ikiisha kumea, huwa kubwa kuliko mimea yote, ikawa mti, hata nyuni wa angani huja na kukaa katika matawi yake" (Mathayo 13:31-32).

NENO la MUNGU kwa imani linapojiimarisha kwenye moyo wa mtu, linakuwa mti mkubwa, kwa sababu mtu mwenye imani huanza kulitangaza NENO la MUNGU kwa upeo na mapana, na kanisa linakuwa kutoka kwake. Hata hivyo, kanisa linapokua, linakuwa makazi ya watu wengi. Baadhi ya watu wenye mapepo hujipenyeza kuingia kanisani, wakijaribu kuliharibu kwa kupanda mafundisho ya uongo na kufanya mashitaka ya uongo kwa wazee ikiwa ni utii wao kwa Shetani.<sup>15</sup>

Mapepo katika mfano huu wamefananishwa na ndege wa angani ambao huja na kukaa katika matawi yake. Wamo katika kila kanisa la kweli. Kazi ya Shetani ni kuzuia kazi ya MUNGU kwa kila njia ajuayo, na anajua njia nyngi tofauti-tofauti.<sup>16</sup> Amekuwa na uzoefu wa miaka 7,000. Hii ndio sababu tunalazimika kuwa na nia ya KRISTO (1 Wakorintho 2:16) na silaha zote za MUNGU (Waefeso 6:11) ili tuweze kuzipinga hila za Shetani.<sup>17</sup> 1 Petro 5:8 inasema, "Muwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze." Kwa hiyo, "Basi mtiini MUNGU,

## Missouri

Mpendwa Mchungaji Alamo,

Neema na upako wa Mungu ambao unapita ufahamu wote na maarifa kuititia Mwanawe Yesu Kristo uwe juu ya huduma yako. Nilipiga simu mwezi Novemba kushuhudia mstari wa maombi kwa ajili ya mke wangu; ana saratani. Nimeshughulika sana na matatizo ya moyo. Maombi yenu ni msaada sana kwangu na familia yangu. Naomba kila siku na usiku kwa ajili ya wapendwa wangu na Mchungaji Alamo. Umekuwa msaada sana kuniruhusu kufikia kiwango cha juu cha uelewa wa kiroho. Najua kwamba roho yangu imebadilishwa kwa Bwana kwa nyenzo ambazo umenitumia. Nimewaambia ndugu zangu kuhusu wewe. Asante sana kwa msaada wako. Naomba kwamba Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo aniachilie kutoka kwenye gereza hili. Kesi yangu ya msamaha itakuwa tarehe ijayo Februari. Pia nakuombea uachiliwe hivi karibuni vile vile.

Robert Green

Farmington, MO

Mpingeni Shetani, naye atawakimbia" (Yakobo 4:7).

Inaonekana kuwa kazi ya kuchosha kwa watu ulimwenguni kujiokoa wenyewe kutoka kwenye uharibifu wa ulimwengu huu wa sasa. Wanona ni vigumu kuelekeza akili zao kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, KRISTO pamoja na BABA YAKE ambao wanaketi juu yake, na ROHO saba za MUNGU, ambazo ni macho ya MUNGU kama ilivyoolezwa katika kitabu cha Zekaria, sura ya 4, mstari wa 10: "hizi saba [ROHO za MUNGU] ndizo macho ya BWANA; yapiga mbio huko na huko duniani mwote." Pia, Isaya 11:2 inaelezea majina ya ROHO saba za MUNGU, ambazo ni 1) ROHO ya MUNGU, 2) ROHO ya hekima, 3) ROHO ya ufahamu, 4) ROHO ya shauri, 5) ROHO ya uweza, 6) ROHO ya maarifa, na 7) ROHO ya kumcha BWANA.

Ufunuo 1:4 inasema, "Yohana, kwa yale makanisa saba yaliyoko Asia [Uturuki]; Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwake YEYE aliye ko na aliye kuwako na atakayekuju; na zitokazo kwa ROHO saba waliko mbele ya kiti chake cha enzi." Na Ufunuo 3:1 inasema, "Haya ndiyo

anenayo YEYE [YESU] aliye na hizo ROHO saba za MUNGU, na zile nyota saba."

Kwa mahangaiko yote ya dunia, unawezakosa ufahamu wa ukweli kwamba MUNGU anajua kila kitu kinachoendelea ulimwenguni mwote, au kuwa ROHO WAKE anajua hasa kile unachofikiri na mahali ulipo. Anajua kila jambo kukuhusu.<sup>18</sup> Tatizo ni kwamba hujui kuwa MUNGU anamimina mto WAKE wa UZIMA, ROHO WAKE wa UZIMA, juu yako ili uvipokee kama UZIMA wako wa milele. Una mai-sha ya kidunia, ambayo yatakoma hivi punde, labda mapema kuliko udhaniavyo. Hata hivyo, MUNGU anataka upokee UZIMA WAKE wa milele katika roho yako ya milele ya kibinadamu ili uweze kuishi NAYE milele Mbininguni.

Unao mwili, nafsi, na roho. Biblia inasema kwamba mwili haufai kitu (Yohana 6:63), na nafsi itendayo dhambi inapaswa kutengwa, ila roho yako – kama unataka UZIMA wa milele – ni lazima upokee ROHO ya KRISTO ya UZIMA wa milele ndani yake. Mto wa UZIMA wa milele unakusubiri upokee UZI-  
(Inaendelea ukurasa wa 8)

<sup>15</sup> Dan. 11:30-32, Mat. 7:13-23, 10:16-18, 21-28, 13:24-31, 36-43, 47-50, 24:9-12, Mdo. 20:28-31, Gal. 2:3-5, 2 Pet. sura ya. 2, 1 Yoh. 2:18-19, 4:1-6, 2 Yoh. 7-11, Yud. 3-19 <sup>16</sup> Isa. 14:4-20, Mat. 24:24, Yoh. 8:44, 10:10, 2 Kor. 4:3-4, 11:13-15, 2 Thes. 2:3-12, 1 Pet. 5:8, 1 Yoh. 4:1, Ufu. 2:9, 12:9, 13:1-8, 11-14, 16:13-14, 20:8-15 <sup>17</sup> 1 Kor. 2:11-16, 15:57-58, 16:13, 2 Kor. 6:1, 4-7, 10:3-6, Efe. 4:27, 6:10-18, Fil. 2:5, 1 Thes. 5:3-9, 21, 1 Tim. 6:12, 2 Tim. 2:3-4, Ebr. 4:12, 12:1-4, Yak. 4:7, 1 Pet. 5:8-10, 1 Yoh. 5:4 <sup>18</sup> Kumb. 31:21, 1 Sam. 16:7, 2 Fal. 19:27, 2 Nya. 16:9, Zab. 7:9, 66:7, 139:1-6, 12-16, Isa. 29:15-16, 46:9-10, 48:5, Yer. 1:5, Amo. 9:1-4, Lk. 12:2-7, Rum. 8:27-29, 1 Yoh. 3:20

# USHUHUDA WA TERRI WHITE

## Mujiza wa Ukombozi

Sikutoka kwenye nyumba iliyovunjika ikiwa imezungukwa na machafuko, kuchanganyikiwa, pombe, au madawa ya kulevyta, lakini nilikuzwa na wazazi wenye upendo, wenye kusaidia ambao walijitoa maisha yao kwa ajili ya kaka yangu na mimi. Tulizoea furaha ya utotoni, uvuvi, kuendesha farasi, kupiga kambi na kuteleza juu ya maji siku za mwisho wa juma.

Haikuwa mpaka Krismasi yangu ya nane ambapo nilipokea Biblia yangu ya kwanza kutoka kwa bibi yangu. Nikiwa najua kuwa kilikuwa kitabu maalumu, nilijipangia ratiba binafsi na kusoma kwa shauku kuu. Hiki hakikuwa kitabu cha hadithi kuhusu Yesu. Matokeo ya ajabu ambayo Yesu aliwapa wanadamu walio-kuwa wakiteseka, miujiza aliyoifanya, tumanini na amani aliyowaachia watu, vilinifanya nitafakari, "Oh! Kama ningeweza kuishi basi, ningemuata Yesu." Kisha nikazama katika dimbwi la kukata tamaa kwa sababu huyu Yesu wa Biblia hakuwa dhahiri katika dunia hii niliyoishi.

Baba yangu alipitia matukio ya kushusha moyo sana kupitia viongozi wa dini, na hakwenda kanisani kamwe, hadi baada ya wokovu wangu miaka mingi baadaye alipokuja kwenye Wakfu wa Kikristo wa Tony na Susan Alamo. Hivyo, kaka yangu na mimi tulipelekwa kwenye shule ya Jumapili na kuachwa hapo. Uzoefu wangu mdogo wa kanisa la Kibaptisti ulikuwa kwamba ni lazima tuokoke, nilidhani, kutoka kuzimu. Watu wabaya kama majambazi, wauaji, waonevu, nk., watakwenda huko, si watu kama sisi. Nilijishughulisha binafsi na uendeshaji farasi wa aina ya palomino katika magwaride ya manyesho. Alikuwa na uhakika wa kushinda na kuvutia watu wengi sana! Siku moja nikiwa njiani kwenda kwenye gwaride kubwa, tulipata ajali na farasi

wangu, Amigo, aliuawa. Nilivunjika-vunjika; ndoto zangu zikatoweka. Ingenichukua muda kabla ya kujihusisha na farasi tena.

Marafiki wangu shulen i walinishawishi kutoka kila upande kuijingiza kwenye ulimwengu unaokua kwa kasi wa madawa ya kulevyta na madawa yenye kuleta njozi. Baada ya mahafali yangu ya kuhitimu shule ya sekondari, wazazi wangu walituhamishia kwenye mazingira bora zaidi. Tulihamishiwa katika milima ya Rocky ya Colorado karibu sana na mto wa Little Cimarron. Tulikuwa tumezungukwa na maziwa, mito, milima, na uwanda kila upande wetu. Nyumba ya kulala ya wageni wawindaji ya jirani yetu ilikuwa ng'ambo ya ziwa, na ilikuwa maarufu kwa uwindaji na uvuvi. Nilajiriwa katika nyumba hiyo kama mwongoza misafara ya farasi. Nilitumia masaa kutunza farasi wa Nyumba ya wageni ambao walitumika kwa ajili ya safari za uwindaji. Siku moja mahususi nilipokuwa nikiendesha farasi peke yangu, nilifika sehemu ya juu zaidi ya Uwanda wa juu wa Magharibi. Nilipokuwa nikitazama mandhari kuu, nilishangazwa na miti ya aspen yenye majani ya dhahabu, ilijojisokota, yenye harufu nzuri ya msonobari, kichaka cha rangi ya chungwa na mito imiminikayo, ungeweza kuisikia harufu safi. Maswali haya yaliniwinda: Uzuri wote bora namna hii Mungu ameumba, lakini kwa nini sikuwa na uzuri huu ndani yangu? Kwa nini fikra zangu na tamaa zangu ni mbaya, mbinafsi na oyoo? Kwa nini ilionekana kama vile nilikuwa na mnyama mbaya wa porini ndani yangu? Nilibaki nimechanganyikiwa nikiwa tu na maswali zaidi.

Bila kujizuia au kuwa na wazo, nilikuwa nimewakosea na kuwatumia



Dada Terri White

watu wote walionipenda. Niliondoka na sikuangalia nyuma. Mwaka ulio-fuata kwa kiasi nilipoteza mawasiliano na ulimwengu mbaya ulionizunguka. Sikuona kitu cha kuyakabidhi maisha yangu au kuyajenga juu yake. Bila malengo nilihama kutoka mji moja hadi mwingine, jimbo moja hadi jingine, kutoka kwenye sherehe moja ya madawa kwenda kwenye nyingine. Nilitumia pombe ya kutosha na vidonge na bangi kuua utu wangu wa kawaida. Lakini mwamko halisi ulikuja baada ya mfutano wa matukio ambayo yalinishtua toka kwenye uzubavu wangu. Kwa namna fulani nilinusurika nilipozidisha madawa ya kulevyta, mlipuko wa moto, ajali ya boti na kutekwa wakati nilipope-wa lifti ya gari. Na pia nilipona katika ajali nilipomshikia bunduki mtu ambaye alimpiga kaka yangu. Tukio hili la mwisho lilikuwa mapambazuko ambalo lilinifanya nitambue kwamba nilikuwa nimeshindwa kujitawala. Kwa hakika Mungu alikuwa na hasira na mimi na nilijua nilikuwa nikielekea. Jehannamu moja kwa moja. Jinsi gani ningeweza kufuta kile nilichokifanya mwenywewe na maisha mengine niliyoharibu?

Nilikuja Hollywood, CA, kwa lengo moja ambalo lilikuwa kutengeneza

pesa na kisha kwenda milimani kujaribu kujificha kutoka kwenye ukali halisi ulionizunguka. Nilichukia jiji na hususan Hollywood. Nilijua mara tu nilipofika hapo kwamba nilikuwa nimefanya makosa makubwa kwenda huko. Fedha nilizokuwa nimetengeneza ziliibowi, na kiburi changu kilinizuia kuwapigia wazazi wangu simu. Niliogopa mno kuomba lifti; nilinaswa kama panya. Wiki iliyofuata katika Sunset Strip, nilikutana na kundi la vijana wadogo ambaao walionekana kama kila mtu mwengine, lakini lengo lao lilikuwa tofauti kabisa na la watu wengine. Watu wa mtaani walikuwa wakiwadhihaki na kuwaita "Kikosi cha Mungu." Wakati watu hawa hawa walipozungumza na mimi, waliongea kwa mamlaka na kujali kwa kweli. Sikuweza kuepuka dharura ya ujumbe wao. "Yesu anarudi duniani. Tubu au upotee. Fanya amani na Mungu wakati ungalipo. Yesu anarudi duniani akiwa na fimbo ya kisasi dhidi ya wale wote ambaao hawamjui. Jehannamu ni ya milele. Tunaishi katika siku za mwisho. Sawazisha uhusiano wako na Mungu kabla hujachelewa. Njoo kwenye huduma za kanisa tulizo nazo kila usiku na ufahamu mengi zaidi."

Neno "Jehannamu" lilinigonga kwa nguvu kwa sababu nilijua ilikuwa kweli. Lilikuwa kwenye mawazo yangu kwa ukubwa na uwazi. Mara kitu fulani ndani yangu kilisema, "Daima ulisema ni mtafutaji wa kweli. *Nenda utafute kuhusu hili.*" Yapata juma moja baa-daye nilipata usafiri wangu mwenyewe na nikaja kwenye huduma ya kanisa katika Crescent Heights Blvd. katika Hollywood. Ilikuwa Novemba 9, 1970. Iliitwa Tony and Susan Alamo Christian Foundation. Sikuweza kukataa nguvu, Roho ilazimishayo ikinivuta, licha ya mashaka na wasiwasi uliojaa na kujificha akilini na moyoni wangu. Haya yalikuwa majibu ya asili dhidi ya kashfa, uongo, na unyanyasaji wa binadamu ambayo kwayo nilijeruhiwa. Bila msaada niliupora ujana wangu,

nilikuwa mada ya hadithi ya kutisha. Nilijilaumu mwenyewe kwa maamuzi mabaya niliyochagua kufanya.

Nilipoingia kwenye jengo kubwa, la ghorofa mbili lililokuwa limejawa na watu walioonekana kama Wahipi, ilikuwa na hisia za furaha na shauku ya dhati ambayo ilikuwa dhahiri kwan-gu. Mchungaji Tony Alamo alione-ka-na kuwa wa pekee mahali pale akiwa mionganii mwa Wahipi, akiwa ameva-llia suti ya kazi. Nilikuwa nimekusudia kumwangalia kwa makini na kila kitu atakachosema. Sikukutana na mkewe Susan usiku ule. Huduma ilianza moja kwa moja kwa kuimba nyimbo za nyakati za kale za injili. Mtu alicheza "Ni mtoto gani huyu" kwa zumari, na ilionekana kana kwamba melodi hii ya kimalaika ilikuwa ikitoka mbin-guni. Hapakuwa na okestra iliyokuwa ikifuatana na melodi, lakini kitu fulani kilikuwa kikizidi nguvu kinga ya ulinzi niliyokuwa nimejenga kuuzungu-ka moyo wangu. Machozi yalikuwa yakinirika usoni mwangu, na nilikuwa nikipata uzoefu wa huduma ya kwanza iliyojazwa kwa Roho Mtakati-fu maishani mwangu. Nilikuwa mwenye dhambi aliyepotea ambaye aliqui-wa anakwenda kupatikana. Waumini wapya waliookolewa walitoa shuhuda fupi, lakini zinazozieleza. Lazima kuli-kuwa na shuhuda 100 usiku ule. Kuli-kuwa na wawakilishi kutoka Ufaransa, Uingereza, Canada, Australia, Mexico, Amerika ya Kusini, karibu duniani kote. Pia kulikuwa na watu wazima wenye umri wa kati ambaao waliali-cha makanisa yao baridi, yaliyokufa kujiunga na mwendo maalaumu wa Mungu. Kila moja ya shuhuda zao ulikuwa muhimu kuanzisha matumaini na imani ndani yangu, na kumenya tabaka baada ya tabaka la mashaka na uonevu liliozunguka moyo wangu na nafsi. Nilisikia kuhusu wazoefu wakubwa wa madawa ya kulevyia na wauzaji madawa ya kulevyia wakikombolewa papo kwa hapo kwa nguvu ya Mungu iokoayo, na kuhusu wal-

evi kuja bila weweseko la ulevi. Mtu mmoja aliyejikuwa njiani kwenda kuiba benki alipoacha na kuletwa kanisani alizaliwa kwa mara ya pili, na akafany-wa kiumbe kipyga baada ya kumkubali Yesu kama Bwana wake.

Mchungaji Alamo alileta ujumbe kuhusu unabii wa nyakati za mwisho na kusoma toka sura ya 24 ya Mathayo. Ulikuwa ni urahisi wa injili, injili ya maarifa ya kawaida, akihubiri kwa nguvu za Roho Mtakatifu wa Mungu. Ningeweza je kupinga mwaliko wa kupiga magoti mbele ya madhabahu na kumwomba Yesu kuingia ndani ya moyo wangu? Mchungaji Tony pia alipiga magoti chini vile vile na akan-iongoza kusali sala ya toba kulingana na Biblia Takatifu. Baada ya kutubu na kumwomba Yesu kuosha dhambi zan-gu kwa damu yake ya thamani, na kum-walika moyoni mwangu, Alinisamehe! Nilikuwa mpya! Uwepo wa kutokuwa na hatia wa imani kama ya mtoto uli-jaza moyo wangu. Furaha, amani, na tumaini vilinijaza na kufurika, kupita matarajio yangu makubwa. Nilifany-wa kuwa kiumbe kipyga. Nilielewa na nilionja nguvu iokoayo, muujiza wa ukombozi, ambaao Yesu pekee ndiye awezaye kutoa. Mtu huyu wa muujiza wa Biblia yangu ya kwanza kama mtoto anaishi na anafanya kazi, anaongea na kutembea na wale wote ambaao wan-afungulia mlanga wa moyo wao.

Ni zaidi ya miaka 42 ambayo nime-shuhudia na kupata uzoefu wa up-onyaji, kufufuka, na nguvu ya kuokoa. Nimeona miujiza mingi nisiyoweza kuweka katika hesabu hii. Haya ni matokeo ya Mchungaji Tony na mare-hemu mkewe Susan Alamo kwa kiasi kikubwa kujitoa maisha yao wenywewe kushinda roho na kuziotesha mizizi na kuzipanda katika Neno Takatifu la Mungu. Wametufundisha mitego ya uongozi wa Shetani na kumweka wazi Mpinga Kristo kwa mapana. Nashuku-ru milele. Utukufu uwe kwa Mungu, na muamana ziende kwa mpendwa wetu Mchungaji Tony Alamo.

## KRISMASI NI WOKOVU

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 5)

MA, ambao upo ndani ya KRISTO YESU. Hivyo sema sala hii:

BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mwenye dhambi<sup>19</sup> ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.<sup>20</sup> Ninaamini kwamba alikufa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.<sup>21</sup> Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kuitia nguvu za ROHO MTAKATIFU<sup>22</sup> na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikiliza maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.<sup>23</sup> Ninfungua mlango wa moyo wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.<sup>24</sup> Nioshe dhambi zangu kwa damu ulioimwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,<sup>25</sup> hutnikataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia linasema hivyo.<sup>26</sup> NENO LAKO linasema hutnikataa yeote na

mimi nikiwemo.<sup>27</sup> Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.<sup>28</sup> Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuo-ko-ko roho yangu na nitaonesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kutotenda dhambi tena.<sup>29</sup>

Baada ya kuokoka YESU alisema ni lazima kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa kwenye maji mengi kwa jina la BABA, MWANA na ROHO MTAKATIFU.<sup>30</sup> Kwa makini soma Biblia ya KJV, tafsiri ya Kiswahili ya The Bible League, Waenezaji wa Neno la MUNGU tangu 1938 na ufanye inavyosema.<sup>31</sup>

Kama unapenda kumtumikia BWANA, unaweza kufanya hivyo katika kanisa letu kama ukizishika sheria.

Kisha, kama anavyoamuru YESU, kuwa muongoaji roho. Unaweza kufanya hivi kwa kuwa msambazaji wa maandiko ya Mchungaji Alamo. Tunachapa maandiko ya Mchungaji Alamo katika lugha nyingi, na kuyapeleka kote ulimwenguni. Tunatumia mamilioni ya dola kwenye karatasi na usafirishaji, hivyo tunahitaji sala zako na msaada wa kifedha.

Iwapo unataka dunia yote iokolewe, kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, “Je! Mwanadamu atamwibia

Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghalani, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mb-inguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeze alaye, wala hataharibu mazao ya ardhii yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi” (Malaki 3:8-12).

MUNGU anatuamuru kuwasahihi-sha na kuwaadhibu watoto wetu.<sup>32</sup> Ndoa imeruhusawa na MUNGU katika umri wa kupevuka wakati ambapo watoto wanakuwa wanaume na wanawake. Kuzuia hili ni mafundisho ya Shetani (1 Timotheo 4:1-3). Mchungaji Alamo yupo gerezani kwa kuhubiri kile isemacho Biblia.

**19** Zab. 51:5, Rum. 3:10-12, 23 **20** Mat. 26:63-64, 27:54, Lk. 1:30-33, Yoh. 9:35-37, Rum. 1:3-4 **21** Mdo. 4:12, 20:28, Rum. 3:25, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 5:9 **22** Zab. 16:9-10, Mat. 28:5-7, Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21, 10:17-18, 11:25, Mdo. 2:24, 3:15, Rum. 8:11, 1 Kor. 15:3-7 **23** Lk. 22:69, Mdo. 2:25-36, Ebr. 10:12-13 **24** 1 Kor. 3:16, Ufu. 3:20 **25** Efe. 2:13-22, Ebr. 9:22, 13:12, 20-21, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 1:5, 7:14 **26** Mat. 26:28, Mdo. 2:21, 4:12, Efe. 1:7, Kol. 1:14 **27** Mat. 21:22, Yoh. 6:35, 37-40, Rum. 10:13 **28** Ebr. 11:6 **29** Yoh. 5:14, 8:11, Rum. 6:4, 1 Kor. 15:10, Ufu. 7:14, 22:14 **30** Mat. 28:19-20, Yoh. 3:5, Mdo. 2:38, 19:3-5 **31** Yos. 1:8, 22:5, Zab. 1:1-2, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Yak. 1:22-25, Ufu. 3:18 **32** Mit. 13:24, 19:18, 22:6, 15, 23:13-14, 29:15, 17, Ebr. 12:5-11, Ufu. 3:19

*Tafadhali wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambazo unaweza kuvutiwa nazo:*

**Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078**

**Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362**

**www.alamoministries.com • info@alamoministries.com**

*Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani ambao wanataka kumtumikia BWANA kwa miyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.*

**Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.**

**Tafadhali wasiliana nasi kuitia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.**

*Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kiiwach, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO  
alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.*

*Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo  
Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kuitia meli.*

*Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhali tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.*

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)  
USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

**Kwa wale ambao mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo  
mtachapisha tena, tafadhali jumuisha haki hii na usajili:**